LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA ZA USALAMA BARABARANI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# SHERIA ZA USALAMA BARABARANI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

**SHUKRANI** .......... **6**
**DIBAJI** .......... **6**
**1. MAANA YA SHERIA ZA BARABARANI** .......... **10**
**1.1.Baadhi ya Alama za Barabarani** .......... **11**
**2. USAJILI WA GARI** .......... **11**
**2.1.Hati ya Usajili wa Gari** .......... **12**
**3. LESENI YA KUENDESHA GARI** .......... **14**
**3.1.Maana ya Leseni** .......... **14**
**3.2.Madaraja ya Leseni na Taratibu za Upatikanaji wa Leseni za Udereva** .......... **15**
3.2.1. Madaraja ya Leseni za Udereva .......... 15
3.2.2.Umri wa Madaraja ya Leseni .......... 17
3.2.3.Leseni ya Kujifunzia (Learner's Driving lisence) .......... 18
3.2.4.Utaratibu wa Kuomba Leseni za Udereva kwa Madaraja Mengine kwa Dereva Mpya .......... 18
3.2.5.Kubadilisha Daraja la Leseni .......... 20
3.2.6.Kubadilisha Madaraja ya Leseni .......... 22
3.2.7.Utoaji wa Leseni za Udereva kwa wenye Ulemavu wa Maumbile ya Mwili .......... 24
3.2.8.Utaratibu wa Kupata Leseni ya Udereva Iliyopotea (Duplicate) .......... 24
3.2.9.Leseni za Kimataifa .......... 25

3.2.10.Kunyang’anywa Leseni....................................................................26

3.2.11.Ajali...................................................................................................27

**4. UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USALAMA BARABARANI ......... 28**

4.1.Majukumu ya Askari wa Usalama Barabarani ...........................28

4.2.Makosa yaliyoainishwa na Sheria ya Usalama Barabarani 29

4.3.Adhabu za Makosa ya Usalama Barabarani...............................30

4.4.Taratibu za Mashauri ya Makosa ya Usalama Barabarani ..30

4.5.Taratibu za Uendeshaji wa Mashitaka ..........................................31

**5. Kanuni ya Usalama Barabarani juu ya uwekwaji wa alama za viakisi mwanga katika magari ya mwaka 2015 [The Road Traffic (Motor Vehicle Retro Reflective Markings) Regulations, 2015] .. 34**

**6. HITIMISHO ..........................................................................................35**

## SHUKRANI

Tunatoa shukurani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususan Wakili Shilinde Ngalula, Wakili Hamisi Mkindi, Wakili Hamisi Mayombo, Wakili Veneranda Joseph, Frida Eligius na Ndugu Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, hususan wa Kituo cha Arusha.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa

kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inaababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.
Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiaa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

# LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. MAANA YA SHERIA ZA BARABARANI

Hii ni sheria ambayo inalinda matumizi mbali mbali ya barabarani na kutoa maelezo sahihi kuhusu sheria za barabarani. Sheria hii inatoa maelezo kuhusu makosa ya barabarani na adhabu zake, vile vile sheria hii inaeleza kuhusu taratibu za usajili wa gari pamoja na namna ya kupata leseni halali za kuendesha magari zikiwa zimegawanyika katika madaraja mbali mbali. Sheria hii inaeleza zaidi kuhusu uvunjifu wa sheria za barabarani na adhabu zake kwa makosa mbali mbali ya barabarani. Sheria hii pia inatoa mwanga kwa watumiaji wote wa barabara na namna ya matumizi halali ya barabara. Sheria hii inaitwa Sheria ya usalama Barabarani sura ya 168 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Ni muhimu kwa kila mtumiaji wa barabara kufahamu sheria hii na kuelewa namna ya matumizi bora ya barabara, kwa nia ya kuepuka kuvunja sheria pamoja na kuepuka ajali kutokana na matumizi mabaya ya barabara.

### 1.1. Baadhi ya Alama za Barabarani

Ni muhimu kwa kila mtumia barabara kufahamu na kuzingatia alama mbali mbali za barabarani alama hizi ni pamoja na alama za vivuko vya waenda kwa miguu, alama za waendesha baiskeli, alama za maandamano au mikusanyiko barabarani, alama za makundi ya wanyama, alama za mwendo kasi wa ziada, alama za kufungwa kwa barabara, alama za maeneo ya maegesho ya magari, alama ya njia moja (one way) itokayo au iingiayo n.k.

# 2. USAJILI WA GARI

Sheria ya Usalama Barabarani inaelekeza kwamba kila gari linatakiwa kuwa limesajiliwa kwa Msajili ndipo liruhusiwe kutembea barabarani. Ni kinyume cha sheria kwa mtu yoyote kuendesha gari ambalo halijasajiliwa. Endapo mtu yeyote atakaidi na kuendesha gari lisilo na usajili, mtu huyo atakuwa amevunja sheria na adhabu yake ni faini au kifungo gerezani au kutumikia adhabu zote kwa pamoja.

Si ruhusa kwa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 kusajiliwa kama mmiliki wa gari. Sheria hii pia inaruhusu mtu mwenye umri wa miaka 14 kupewa usajili wa kuendesha pikipiki. Vile vile sheria hii inakataza mtu yeyote mwenye matatizo ya akili kupata usajili wa gari.

Msajili atasajili gari baada tu ya kujiridhisha kwamba gari lipo kwenye hali nzuri ya kuweza kutembea barabarani. Kabla ya kupatiwa usajili, mnunuzi atatakiwa kukamilisha malipo yote ya gari husika; baada ya kujiridhisha msajili atasajili gari hilo kwa jina la mhusika na pia atatoa namba mpya ya usajili wa gari husika. Endapo gari litakuwa chini ya umiliki wa mtu zaidi ya mmoja, gari hilo litasajiliwa kwa jina au majina ya wamiliki husika. Vile vile hati moja ya gari haitatumika kama hati ya magari mengine ya mhusika. Kila gari litatumia hati inayojitegemea. Mamlaka ya Mapato Tanzania (T.R.A) ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia usajili wa magari na vyombo vingine vya moto nchini Tanzania.

### 2.1. Hati ya Usajili wa Gari

Hati halisi au kivuli cha hati hiyo ya usajili wa gari inatakiwa kwa muda wote kuwapo ndani

ya gari na ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kuendesha gari bila hati ya usajili wa gari au kivuli cha kadi kilichothibitishwa na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA). Adhabu ya kosa hili ni kifungo cha jela au faini ya fedha au adhabu zote kwa pamoja. Mtu ambaye jina lake litakuwa limetumika kwenye usajili wa gari, basi mwenye jina hilo ndiye atakaye julikana kama mmiliki halali wa gari husika.

Nyaraka na vitambulisho vyote vya gari lazima viwemo ndani ya gari kwa muda wote na vitanakiwa kuwekwa sehemu ambayo vitaonekana na kutambuliwa kwa urahisi.Endapo dereva atavunja sheria hii, adhabu yake ni faini au kifungo jela au adhabu zote kwa pamoja.

Endapo mmiliki halali wa gari atataka kubadili umiliki wa gari, anaruhusiwa kufanya hivyo siku saba baada ya usajili wa mwanzo na atafanya hivyo kwa kurudisha hati ya kwanza ya usajili kwa msajili; na hii ni baada ya kuonyesha mkataba halali wa kubadili umiliki wa gari husika.

# 3. LESENI YA KUENDESHA GARI

## 3.1. Maana ya Leseni

Leseni ni hati ambayo inamtambulisha dereva wa gari au pikipiki au chombo kingine cha moto kuwa amepitia mafunzo na kufaulu na kwamba ana uwezo na vigezo vyote vya kuendesha gari; pikipiki au chombo chochote cha moto. Leseni zimegawanyika katika makundi tofauti kutokana na aina ya gari, pikipiki au chombo kingine cha moto.

Sheria ya Usalama Barabarani inazuia mtu kuendesha aina yoyote ya gari au chombo chochote cha moto barabarani bila ya kuwa na leseni halali au hati ya mafunzo ya kuendeshea gari. Vile vile ni kinyume na sheria kwa mmiliki wa gari kugawa/kuruhusu gari kwa mtu asiye na leseni halali ya kuendesha gari. Ni muhimu kufahamu kwamba leseni zimegawanyika katika madaraja tofauti kutokana na aina za magari na/au vyombo vya moto husika.

Kwa mtu anayejifunza kuendesha gari au chombo chochote cha moto akiwa katika shule

ya udereva, atalazimika kuomba hati maalumu ya mafunzo ya kuendesha gari au chombo cha moto husika ambapo hati hiyo inadumu kwa muda wa miezi mitatu. Gari linaloendeshwa na mtu aliye mafunzoni litatambulika kwa kuonyesha alama maalumu (alama L). Mtu atakaye hitimu mafunzo ya kuendesha gari, atapokea cheti kitachoonyesha kuwa ni mhitimu wa mafunzo hayo. Baada ya hapo, atawasilisha cheti hicho katika mamlaka husika (TRA) ili aweze kupatiwa leseni.

## 3.2. Madaraja ya Leseni na Taratibu za Upatikanaji wa Leseni za Udereva

### 3.2.1. Madaraja ya Leseni za Udereva

1. Daraja A.Pikipiki zenye ukubwa wa zaidi ya 125cc au uzito wa 230kg na kigari cha pembeni au isiyokuwa na kigari;
2. Daraja A1. Pikipiki zenye ukubwa wa chini ya 125cc au uzito wa 230kg na isiyokuwa na kigari cha pembeini;
3. Daraja A2. Kuendesha pikipiki za magurudumu matatu au manne;

4. Daraja A3. Mitambo ya kukatia majani au pikipiki zisizozidi 50cc;
5. Daraja B. Magari aina zote (Private vehicles) isipokuwa magari ya biashara (Commercial), magari ya kubeba abiria (PSV), magari ya makubwa ya (HDV) na Pikipiki;
6. Daraja C. Magari ya akubeba abiria kuanzia 30 na zaidi;
7. Daraja C1. Magari ya kubeba abiria 15 hadi 29;
8. Daraja C3. Magari ya kubeba abiria hadi 14;
9. Daraja C3. Magari ya abiria wasiozidi wanne;
10. Daraja D. Magari ya aina zote isipokuwa magari ya abiria (PSV), magari makubwa ya mizigo (HDV) na pikipiki;
11. Daraja E. Magari ya aina zote isipokuwa magari ya abiria (PSV) na pikipiki
12. Daraja F. Mitambo kama Graders, Folklift n.k;

13. Daraja G. Mitambo ya mashambani na migodini kama trekta; n.k.
14. Daraja H. Leseni za kujifunzia kuendesha magari (Learner).

### 3.2.2. Umri wa Madaraja ya Leseni

- Daraja A, A1, na A2 - Miaka 18 na kuendelea;
- Daraja A3 – Miaka 16 na kuendelea;
- Daraja B –Miaka 18 na kendelea;
- Daraja C-Miaka 24 na kendelea;
- Daraja C1- kuanzia miaka 21;
- Daraja C2 na C3 –kuanzaia miaka 21 {kwa mujibu wa kanuni za SUMATRA za mwaka 2007 [kif. 17 (2) (b)], dereva mwenye leseni daraja C, C1, na C2 hawezi kuendesha gari la abiria kama ana umri chini ya miaka 30 na asizidi umri wa miaka 60};
- Daraja D- kuanzia miaka 18;
- Daraja E-kuanzia miaka 21;
- Leseini za daraja F na G zitatolewa kwa wenye umri kuanzia miaka 18.

### 3.2.3. Leseni ya Kujifunzia (Learner's Driving lisence)

» Mwombaji anatakiwa awe na namba ya utambuliso ya mlipa kodi (TIN);

» Mwombaji anatakiwa kwenda ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), atapigwa picha, atachukuliwa alama za vildole (vidole vyake kumi), ataweka saini yake kwenye mfumo wa kompyuta (electeronically), Atapewa hati (Payment Notes) ya kutakiwa kulipia leseni hiyo ya kujifunzia (Learner Driving Lisence) katika benki atakayoelekezwa kwa gharama atakayopangiwa kwa wakati husika. Baada ya malipo hayo, atatakiwa kupeleka stakabadhi ya malipo ofisi za mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya kupatiwa leseni ya kujifunzia.

### 3.2.4. Utaratibu wa Kuomba Leseni za Udereva kwa Madaraja Mengine kwa Dereva Mpya

- Dereva atawajibika kuhitimu mafunzo ya udereva katika shule inayotambulika;
- Mwombaji atatakiwa kuwa na leseni ya kujifunzia;
- Mwombaji atatakiwa kwenda ofisi za Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA), atapewa hati (Payment Notes) ya kulipia ada ya majaribio (Test fee-GRR) katika benki na kwa gharama atakayoelekezwa;
- Baada ya malipo hayo atatakiwa kupeleka stakabadhi hiyo ya malipo katika ofisi ya Kikosi cha Usalama Barabarani akiambatanisha na cheti cha mafunzo ya udereva, leseni ya kujifunzia na cheti cha kupimwa macho kutoka hospitali ya serikali au hosipitali inayotambulika;
- Katika hatua hii, mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya kuomba kujaribiwa ambapo atapangiwa tarehe ya kujaribiwa (Maombi haya anaweza kuomba mwombaji mwenyewe au

kupitia chuo cha udereva alichosoma);

- Siku ya kujaribiwa atakwenda Polisi, atajaribiwa kwa gari kulingana na daraja la leseni analoomba;
- Akifuzu atatakiwa kurudi TRA kufanya utaratibu wa malipo ya leseni hiyo na atapatiwa leseni hiyo, yenye kuonesha madaraja aliyofaulu.

MUHIMU

- Watakaobadilisha leseni daraja C kuwa daraja D hawatajaribiwa. Watajaribiwa ikiwa watatiliwa mashaka.
- Watakaogundulika wakiwa na leseni bandia au za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.

### 3.2.5. Kubadilisha Daraja la Leseni

Kupata Daraja E

- Mwombaji anatakiwa awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi.
- Mwombaji atatakiwa aende TRA. Katika hatua hii mwombaji atapigwa picha, atachukuliwa alama za vidole, ataweka

saini.

- Mwombaji atapewa hati (payment note) ya kutakiwa kulipia leseni katika benki atakayoelekzwa na kupeleka stakabadhi TRA kwa ajili ya kupatiwa leseni ya kujifunzia daraja hilo;
- Baada ya mafunzo hayo, atakwenda ofisi za TRA na atapewa hati ya kulipia ada ya majaribio katika benki atakayoelekezwa;
- Baada ya malipo hayo atatakiwa kupeleka stakabadhi hiyo ya malipo ya majaribio Polisi, akiambatanisha na cheti cha mafunzo ya udereva ya daraja analoomba, cheti cha kupimwa macho toka hospitali ya Serikali na awe na leseni daraja D kwa kipindi kisichopunguwa miaka 3 pamoja na cheti cha ushindi (Certificate of Competence); na atatakiwa kujaza fomu ya kuomba kujaribiwa ambapo atapangiwa tarehe ya kujaribiwa;
- Siku ya kujaribiwa atakwenda Polisi,

atajaribiwa kwa gari la kulingana na daraja aliloomba;

» Ikumbukwe kwamba atakayekuwa na leseni ya udereva daraja E, ataruhusiwa kuendesha gari la leseni daraja D.

3.2.6. Kubadilisha Madaraja ya Leseni

1. Kupata Daraja C
   - » Mwombaji atafuata taratibu kama za anayetaka kubadilisha daraja kupata daraja E;
   - » Mwombaji atatakiwa kuwa na leseni ya zamani ya daraja C1 au E yenye zaidi ya miaka mitatu;
   - » Katika hatua hii mwombaji atalazimika kuwa na cheti cha kufuzu kuendesha magari ya usafiri wa umma (PSV) kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) au VETA;
   - » Atafanyiwa majaribio kulingana na gari la abiria

analotarajia kuliendesha na kupata leseni kama maelekezo ya awali yalivyoelekeza;

- Ikumbukwe kwamba atakayekuwa na leseni daraja C, ataruhusiwa kuendesha magari ya leseni daraja C1, C2, C3 na D.

2. Kupata Daraja C1

   - Utaratibu ni kama wa kupata leseni daraja C, tofauti iliyopo ni kuwa mwombaji anatakiwa kuwa na leseni daraja C2, C3 au E.

3. Kupata Daraja C2, C3

   - Utaratibu ni kama wa kupata leseni daraja C, tofauti iliyopo ni kuwa mwombaji anatakiwa kuwa na leseni daraja E au D;
   - Kwa waombaji wa madaraja A, A1, A2, A3, C, C1, C2, C3, E

watajaribiwa upya.

### 3.2.7. Utoaji wa Leseni za Udereva kwa wenye Ulemavu wa Maumbile ya Mwili

- Mwombaji wa leseni ya udereva kwa watu wenye ulemavu, atafuata taratibu za kupata leseni kama waombaji wengine, lakini wakati wa kufanyiwa majaribio, atajaribiwa kwa daraja la leseni kulingana na aina ya gari maalum (Special Motor Vehicle) atakaloendesha kulingana na ulemavu wa maumbile aliyonayo;
- Ulemavu alionao utaonyeshwa kwenye leseni yake; mfano kama anatumia mkono au mguu wa bandia.

### 3.2.8. Utaratibu wa Kupata Leseni ya Udereva Iliyopotea (Duplicate)

- Mwombaji atoe taarifa kituo cha Polisi (cha ngazi ya kuanzia Wilaya) kilicho karibu, atapewa hati ya kupotelewa na leseni (Loss Report);

- Aende ofisi za polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani akiwa na hati ya kupotelewa na leseni, atajaza fomu kueleza sababu ya upotevu wa leseni
- Atatakiwa kwenda ofisi za Mamlaka ya Mapato (TRA) kupatiwa leseni nyingine baada kulipa gharama husika kama atakavyoelezwa.

MUHIMU

Leseni ya zamani ya Duplicate itakubalika katika mchakato wa kubadilisha leseni mpya ikiwa tu mwombaji atakuwa na Cheti cha Umahiri ambacho ni halisi; vinginevyo atapaswa kuanza mchakato mpya.

### 3.2.9. Leseni za Kimataifa

Leseni za kimataifa hutolewa chini ya Mkataba wa Geneva wa 1949 na ule wa Vienna wa mwaka 1968. Leseni hizi hutambulika na kutumika nchini kwa muda usiozidi miezi sita Na ikitokea kwamba mgeni atakuwa nchini zaidi ya miezi sita, atatakiwa kupeleka leseni

aliyokuwa anaitumia nchini kwake Mamlaka ya Mapato Tanzania ili aweze kupatiwa leseni ya udereva ya Tanzania, namba ya hati ya kusafiria itatumika badala ya namba ya utambulisho wa mlipakodi.

### 3.2.10. Kunyang'anywa Leseni

Kwa mtu atakayekuwa amepokonywa leseni kwa kuvunja sheria za barabarani hatoruhusiwa kupata leseni nyingine kwa muda miaka mitatu.

Vile vile ni kinyume na sheria kwa dereva kuhama kutoka kwenye eneo maalumu la kuendesha gari na kuendesha katika eneo lisilo maalum. Muda wowote endapo askari wa barabarani atagundua kuwa dereva wa gari amelewa au ametumia kilevi chochote (kupita kiwango kilichowekwa), atamtaka dereva kuongozana naye mpaka maabara kuweza kupima ili kuweza kujiridhisha kama amekunywa kilevi, na endapo

askari atagundua hivyo atamkamata na kumfungulia mashitaka dereva huyo. Dereva huyo atakaa kituo cha polisi mpaka kilevi kitakapokuwa kimeisha mwilini mwake.

Ni kinyume na sheria kwa mtu yeyote kuendesha gari kwa mwendo kasi zaidi ya ule ulioainishwa kwa gari husika. Ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kumhimiza dereva wa gari kuendesha kwa mwendo kasi kupita kiasi kilichainishwa katika barabara husika.

### 3.2.11. Ajali

Endapo ajali itatokea, ni jukumu la dereva kusimamisha gari na kuangalia kama kuna walioathirika na ajali hiyo na kutoa msaada. Endapo dereva atashindwa kusimama, anatakiwa kutoa taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu na jambo hili lifanyike ndani ya muda wa saa 12 baada ya kutokea ajali hiyo.

# 4. UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USALAMA BARABARANI

## 4.1. Majukumu ya Askari wa Usalama Barabarani

- » Kuhakikisha watumiaji wote wa barabara wanafuata taratibu na kanuni zote za barabarani;
- » Kutunza kumbukumbu za makosa ya usalama barabarani, matukio ya ajali barabarani na kumbukumbu za madereva;
- » Uwezo wa kuwafanyia majaribio madereva wapya na kutoa vyeti kwa ajili ya leseni kwa madereva baada ya majaribio;
- » Uchunguzi na ukaguzi wa magari yanapokuwa barabarani;
- » Kumtaka dereva kuonyesha leseni yake ya udereva pindi anapotakiwa kufanya hivyo;
- » Kuweka gari lenye makosa kizuizini kwenye kituo cha polisi;
- » Kuondoa magari yaliyoharibika barabarani;
- » Kuondoa magari yaliyotelekezwa barabarani au yaliyoachwa kwenye maegesho ya magari;
- » Kutoa amri ya gari kukaguliwa na Afisa Mkaguzi wa Magari wa Polisi wa Kitengo cha

Usalama Barabarani;

- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za mwaka za makosa ya usalama barabarani.

## 4.2. Makosa yaliyoainishwa na Sheria ya Usalama Barabarani

Sheria ya Usalama Barabarani (the Road Traffic Act) kifungu cha 40-42 na kifungu cha 50-51 imeorodhesha makosa yafuatayo:

i. Kusababisha maumivu ya mwili au kifo kutokana na kuendesha gari kwa uzembe, uendeshaji wa hatari au kuwa mlevi aidha wa pombe au kilevi chochote;

ii. Kuegesha au kuendesha gari kwa uzembe pasipo kujali watumiaji wengine wa barabara;

iii. Kuendesha gari kwa mwendo kasi kupita maelezo ya uendeshaji katika barabara husika;

iv. Kushindwa kuheshimu alama za barabarani;

v. Kuyapita magari au vyombo vingine vya moto pasipo kufuata sheria;

vi. Kusimamisha gari eneo lisilo maalum kwa maegesho;

vii. Kumshawishi au kumsaidia dereva wa gari kuvunja sheria.

## 4.3. Adhabu za Makosa ya Usalama Barabarani

Adhabu za makosa zilizoainishwa kwenye Sheria ya Usalama Barabarani kifungu cha 63, ni mbili:

i. Kulipa faini; au

ii. Kifungo.

## 4.4. Taratibu za Mashauri ya Makosa ya Usalama Barabarani

Endapo mtu yeyote atakuwa ametenda makosa kwa kuvunja sheria za usalama barabarani, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la jinai. Taratibu za Mashtaka kwa makosa ya usalama barabarani, yanachukua mkondo wa makosa ya jinai.

Mtu yeyote atakaye thibitika kutenda kosa la usalama barabarani na kosa hilo adhabu yake ni faini, basi Askari wa Usalama Barabarani anayo mamlaka ya kumtoza mtu huyo faini papo hapo pasipo shauri hilo kufikishwa Mahakamani. Makosa yanayoweza kutozwa faini ya papo hapo

ni kama kuendesha gari kwa mwendo kasi, kuzidisha abiria kwa magari ya abiria, kuendesha gari bovu barabarani na makosa mengine madogo madogo.

Endapo mtu atatenda kosa kubwa mfano kumgonga mwenda kwa miguu, ni lazima shauri hilo kufikishwa Mahakamani. Kabla ya kumfikisha Mahakamani, mtuhumiwa atatiwa nguvuni na kuchukuliwa maelezo kwa mujibu wa kifungu cha 11-33 ya Kanuni za Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

### 4.5. Taratibu za Uendeshaji wa Mashitaka

Makosa yote ya sheria ya Usalama barabarani yataendeshwa kutokana na Sheria ya Makosa ya Usalama Barabarani (Road Traffic Act) pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Criminal Procedure Act). Makosa hayo yataendeshwa kwenye Mahakama maalum ya makosa ya usalama barabarani. Ifahamike kuwa Mahakama zote za wilaya nchini zimepewa mamlaka ya kusikiliza na kutoa maamuzi ya kisheria kwa

makosa ya usalama barabarani.

Kwa mujibu wa sheria, mtuhumiwa anapokamatwa na kufikishwa katika Kituo cha Polisi, ni wajibu wa Polisi kumfikisha au kupeleka shtaka lake Mahakamani ndani ya saa 48. Baada ya Polisi kumkamata mtuhumiwa, atalazimika kufanya uchunguzi ili kupata ukweli au maelezo yatakayosaidia kupata ukweli wa kosa au mambo yatakayosaidia kuendesha shitaka kisheria.

Endapo mshitakiwa hatohudhuria Mahakamani, Mahakama itaendelea kusikiliza kesi kwa upande mmoja wa mashitaka na itatoa hukumu bila kujali kutokuwepo kwa mshitakiwa. Vile vile Mahakama inaweza kwa wakati wowote kutoa hati ya kukamatwa mtuhumiwa endapo hukumu itakuwa ni ya kifungo.

Adhabu zinaweza kutolewa bila kufuata mwenendo wa kawaida wa mashitaka Mahakamani. Endapo askari wa usalama barabarani atakapojiridhisha, atatoa notisi ya

hukumu ambapo hukumu hiyo itakuwa kwenye mfumo wa faini na kudumu kwa muda wa siku 28 tangu siku ilipotolewa. Notisi hiyo itaonyesha na kubainisha makosa husika ya mtuhumiwa na kueleza bayana kuwa hakutakuwa na mashitaka mengine Mahakamani dhidi yake. Askari polisi anaweza kumkamata mtu yeyote yule aliyevunja sheria za barabarani bila ya kuwa na hati ya kukamata.

# 5. KANUNI YA USALAMA BARABARANI JUU YA UWEKWAJI WA ALAMA ZA VIAKISI MWANGA KATIKA MAGARI YA MWAKA 2015 [THE ROAD TRAFFIC (MOTOR VEHICLE RETRO REFLECTIVE MARKINGS) REGULATIONS, 2015]

Kanuni zimetolewa chini ya Sheria ya Usalama Barabarani, Kanuni za mwaka 2015 zinazohusu kuwekwa kwa utepe wa viakisi mwanga (reflectors) katika magari zinatafsiri viakisi mwanga kuwa ni utepe unaoakisi mwanga unaoweza kuonekana kirahisi kutoka umbali wa mita elfu moja, utepe unaodumu na kubandikwa kwenye gari husika.

Magari husika yanatajwa kuwa yale ya abiria, magari ya ujenzi, magari ya mizigo mizito yenye ukubwa wa zaidi ya tani 3.5 na magari ya mizigo yasiyozidi tani 3.5

Sheria inataka magari tajwa kubandikwa viakisi mwanga mbele, ubavuni na nyuma ya gari. Zaidi utepe wa kiakisi mwanga unaobandikwa nyuma ya gari unapaswa kuwa wa rangi nyekundu, unaobandikwa ubavuni kuwa wa rangi ya njano na ule unaobandikwa mbele kuwa wa rangi nyeupe.

Utepe wa kuakisi mwanga unapaswa kuwa na upana kati ya milimita 50 na 60.

Sheria inatamka wazi kuwa adhabu kwa atakaye kiuka taratibu za sheria hii, kuwa ni faini ya fedha au kifungo jela au vyote kwa pamoja.

## 6. HITIMISHO

Sheria ya Usalama Barabari ni kati ya sheria muhimu sana katika maisha ya kila siku kwa kuwa watu wote kwa namna moja ama nyingine wanatumia barabara na/au vyombo vya moto. Ni muhimu kwa kila mtumiaji wa barabara kufahamu Sheria za Usalama barabarani kwasababu kutokujua sheria si kinga.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*